

# KICHAACHA MBWA NI HATARI

Kichaa cha mbwa ni ugonjwa wa hatari sana unaoleta vifo kwa binadamu na wanyama. Unadalili zinazoambatana na mishipa ya fahamu ambazo mwanzo huwa ni kuongezeka kwa furaha au hasira, kupoteza fahamu na mwishowe kupooza kwa viungo vya mwili.

Kichaa cha mbwa kimecenza katika sehemu nyingi za dunia. Sehemu za Ulaya ugonjwa huu ultambulikana miaka mingi, kabla 400 BC.

Hapa Tanzania kichaa cha mbwa kilitambulikana mwaka 1932 katika sehemu za Musoma, na Loliondo na kuthibitishwa katika maabarua mwaka 1935 huko Mpwapwa. Hivi sasa kichaa cha mbwa kimecenza katika mikoa yote ya Tanzania isipokuwa mikoa ya Mtwara na Lindi.

## CHANZO:

Chanzo cha Ugonjwa huu ni vijidudu vidogo sana visivoyewa kuonekana kwa darubini vitwawvo Virus. Vijdudu hivi hupatikana katika ubongo, matezi ya mate, mate, kiwele cha maziwa na maziwa ya mnyama aliyeambukizwa.

Mnyama aliyeambukizwa kichaa cha mbwa anaweza kumwambukiza mnyama mwingine siku nne kabla ya dalili za maradhi kuonekana.

Kichaa cha mbwa huambukizwa kwa kuumwa na mnyama aliye na ugonjwa huu. Hata hivyo kuna uwezekano wa kuenezwa na mnyama mwenye kichaa cha mbwa kwa kulamba jeraha la mnyama mzima. Wanyama wanaoeneza ugonjwa huu hasa ni mbwa, mbwa mwitu, mbweha, paka, na wanyama wengine wenye asili ya mbwa na paka.

Wanyama hatari kwa binadamu ni mbwa na paka maana hawa wanaishi nao. Ingawa wanyama wa porini wanawenza kwaambukiza binadamu kwa mfano mbwa mwitu, Mbweha n.k. lakini kwa kuwa binadamu hawakuwazoea wanyama hawa, inakuwa ni vigumu kuwasogeleza.

## DALILI ZA UGONJWA

Baada ya kuumwa na mnyama aliyeambukizwa vijidudu vya kichaa cha mbwa husafiri kupitisha katika mishipa ya fahamu hadi kufikia kwenye ubongo. Ndani ya chembe za ubongo vijidudu hivi hukua na hivyo kuziharibu kabisa chembe za ubongo.

Katika kuzinua kichaa cha mbwa, mbwa huitingwa sindamivinyo dawa wakia na umri wa mmeesi sita.



Muda wa kutokeza ugonjwa huu tangu kuumwa huweza kiuwa siku 10 hadi 12. Maru nyingi muda huu hauzidi miezi mwili, na dalili ya kwanza kabisa huwa ni kubadilika kwa tabia.

Mnyama au mbwa aliye patwa na kichaa cha mbwa mara nyingi hupenda kujificha katika sehemu zenye kiza na hapendi mwanga au kelele. Mwendwa wake hubadilika na kuwa kama wa kuchechemea na huuma vitu visivyoonekana na kubwaka hovyo. Dalili hizi zinaweweza kuendelea na kuwa kichaa kamili

Wakati huu mwanga mkali au kelele humshitunga sana. Hamu ya kula hupungua na mwishowen hushinwa kumeza na kwa kuwa taya la chini huwa limepooza ulimi hutingi na mate hutoka hovyo. Sauti hubadilika na mbwa anaweza kukimbilia maili nyingi akiuma kitu cho chote kipitacho mbale yake. Mwisho huanguka chini katika hali ya kuchoka.

Wakati mwininge mnyama anaweza asonyeshe dalili zote hizou illa akaonvesha dalili za kupooza tu.

Koo hupoza kwanza na mnyama hushindwa kumeza. Sauti yake huwa ni ya kukwaruza.

Baadaye miguu yake hupoza, midomo hukaa wazi ulimi hutoka na kuning inia, mate, huporomoka, macho hutokeza na kuwa kama yana makengeza. Mwishowen mnyama hukaa kimya akiwa amepooza, hukonda na mwishowen hufa. Kifo cha mbwa mwenye kichaa huweza kutokea baada ya siku kumi za dalili za maradhi kuonekana.

Wanyama wa porini wapatwapo na kichaa cha mbwa huwa hawana woga. Huweza kuingia katika mji hata majumbani ambako huuma watu na mitingo hovyo.

Paka wauguapo kichaa cha mbwa huwa wakali zaidi kuliko mbwa. Mata nyingi hushambulia kutoka nyuma na kuumia sehemu za kichwani. Ng'ombe hurusha pembe zake na kutifutatifa udongo kwa miguu yake. Ng'ombe hupata maumivu tumboni, hutoka mate na hupiga kelele hovyo.

## MATIBABU

Mpaka sasa dawa ya kuweza kupoya ugonjwa huu haijaweza kugunduliwa. Inashauriwa kwamba mnyama apatwapo na ugonjwa auwawe mara dalili zigunduliwapo ili asiwe chanzo cha kuambukiza wanyama wengine.

## KUZUIA

Mbwa na paka wawea kupewa dawa ya kuwakinga na kichaa cha mbwa. Paka na mbwa hudungwa sindano ya namna hii wafikapo umri, wa miezi sita na kurudiwa tena baada ya miaka mitatu.

Kinga kwa binadamu ni kujihadhari tu kuumwa na wanyama wanaoweza kuwaambukiza maradhi haya. Ikiwa kwa bahati mbaya utaumwa na mnyama anayeshukiwa kuwa na keihaa cha mbwa, ni vyema kusafisha kidonda kwa maji ya uvuguvugu na sabuni nyingi kisha nenda haraka hospitali.

Ukulima wa kisasa Toleo Na:313 Juni 1982